



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb: Na. HWC/L.20/03/VOL/VIII/86

10.09.2024

MKURUGENZI MTENDAJI,
KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC),
S.L.P 938,
DAR ES SALAAM.

YAH: UTHIBITISHO WA UMILIKI WA ARDHI KWA MWEKEZAJI AGRO MULTI SOLUTIONS LTD KATIKA KIJIKI CHA TALAWANDA HALMASHAURI YA CHALINZE

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

1. Tunapenda kukutaarifu kuwa tarehe 04.7.2024 Ofisi ilipokea barua kutoka kwa Mtendaji wa kijiji cha Talawanda akiitambulisha kampuni tajwa hapo juu ambayo imeonesha nia ya kuwekeza katika kijiji chao ambapo kijiji kilipokea maombi ya kumilikishwa eneo lenye ukubwa wa ekari 431.3 ambazo wamenunua kutoka kwa familia ya Meppo Mbega Wenge.

2. Mtendaji wa Kijiji alieleza kuwa Kampuni ya **Agro Multi Solutions Ltd** ya, **DAR ES SALAAM**, hapa nikiirejea kama Kampuni ya kigeni ambayo inaomba kumilikisha shamba lenye ukubwa wa ekari Mia nne thelathin na moja (**431.3**) kwa ajili ya Kilimo na Ufugaji.

3. Kampuni ya **Agro Multi Solutions Ltd** ilipata eneo hilo kutoka kwa familia moja ya watu 7) katika kijiji cha Talawanda. Kampuni hiyo ililipa stahili za Wananchi hao kwa kuzingatia makubaliano yaliyowekwa kati ya wananchi na kampuni tajwa na baadaye kuwasilisha ombi la umilikishaji kwenye Halmashauri ya kijiji hicho.

4. Baada ya kampuni kukamilisha taratibu za kulipa stahili za wamiliki wa asili, maombi ya kumiliki ardhi hiyo yalijadiliwa na Halmashauri ya kijiji tarehe **04/07/2024** na mapendekezo ya kikao cha Halmashauri ya kijiji yaliwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Talawanda uliofanyika tarehe **12.05.2024** ambapo kwa mujibu wa **Sheria ya Ardhi ya kijiji Na. 5 sura ya 114**, kijiji kilipendekeza mwombaji apewe eneo hilo lenye ukubwa wa **ekari 431.3** ambapo mwekezaji atapaswa kufanya yafuatayo kwenye kijiji:

- (a) Mwekezaji alihaidi kuchimba visima virefu vya maji
- (b) Mwekezaji kuboresha majengo ya shule ya Msingi
- (c) Mwekezaji kutoa kipaumbele kwa ajira zitakazopatikana katika kijiji hicho
- (d) Mwekezaji kuchangia maendeleo ya kijiji

5. Kwa kuwa ukomo wa ugawaji ardhi ngazi za Halmashauri ya kijiji ni ekari 50; Halmashauri ya Wilaya ilipokea muhtasari wa kijiji ukipendekeza kummilikisha mwekezaji **Agro Multi Solutions Ltd** kwa mujibu wa sheria. Baada ya kupokea maombi hayo, timu ya wataalam ilifanya ukaguzi tarehe 22/07/2024 na kubaini yafuatayo:

- (a) Uwepo wa eneo lenye ukubwa wa ekari 431.3
- (b) Eneo hilo halijafanyiwa maendeleo yoyote

6. Kwa sababu hizo, tunapenda kudhibitisha kuwa eneo hilo ni mali ya Kampuni **Agro Multi Solutions Ltd** ambayo imenunua kutoka kwa Wananchi wazawa wapatao 7 wenye jumla ya ekari Mia nne Thelathini na Moja (431), Aidha, tunadhhibitisha kuwa eneo hilo halina mgogoro wowote uliobainika wakati wa ukaguzi.

7. Pamoja na barua hii, nimeambatisha Mikataba ya manunuzi, Mihtasari ya vikao vyote viwili vilivyojadili na kuridhia maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa Sheria

8. Naomba kuwasilisha kwa hatua zinazofuata.



Ramadhani Possi
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
CHALINZE.



Nakala:

✓ Agro Multi Solutions Ltd,
DAR ES SALAAM.

S.L.P 65, CHALINZE 114 Barabara ya Morogoro, 61315 Chalinze Pwani . Simu: +023 32935403,
Nukushi: 023 32935402, Barua pepe: dedchalinze@pwani.go.tz Tovuti: www.chalinedc.go.tz